Kuwatafuta Waliopotea
(Seeking The Lost)

Na

Ellis P. Forsman

Kuwatafuta Waliopotea

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 14, 2011

Kuwatafut a Waliopotea

Luka 19:10

Kazi kubwa ya Yesu Kristo alipokuja hapa ulimwenguni ilikuwa ni kuwaokoa waliopotea.

Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*"

Neno "potea" haimanishi "kutelekezwa" au "kuangamizwa", bali kiufasaa inamanisha "kuwa katika sehemu isiyosahihi." Kamusi ya Vine inaitafsiri kama "ugeni wa kiroho kutoka kwa Mungu." Katika vifungu vingine neno "potea" humanisha "hasara ya uzima wa milele." Kama mtu akibaki katika "sehemu isiyosahihi", na hamrudii Mungu, hakika atajikuta "amepotea milele."

Wakati mwingine tunapojaribu kutafta kitu tunachokiitaji ambayo "imesahaulika" inahitaji juhudi kwa upande wetu ili kuipata. Tunaweza kutoa muda wetu na juhudi ili kuweka sawa kilichopotea.

Yesu alifanya dhabihu kubwa katika kutafuta na kuokoa kilichopotea kwa kutoa uhai wake mwenyewe msalabani ili wengi waweze kuokolewa. Kilicho "*potea*" ilikuwa ni nafsi za wanadamu "zilizosahaulika" katika dhambi za ulimwengu.

Yohana 1:29, "*Siku ya pili yake amwona Yesu akija kwake, akasema Tazama Mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.*"

Kristo hakuja kusuluhisha matatizo ya kisiasa ya Israeli, au kuvunja mgongo wa udhalimu wa Warumi, au kuleta maendeleo katika kilimo, biashara, madawa, au elimu, au kwa kitu kingine kinachofanana na hayo. Alikuja kuwakomboa wanadamu kutoka dhambini.

Alianza katika umri mdogo.

Luka 2:49, "*Akawaambia, kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?*"

Msitari wa 42 inasema Yesu alikuwa na mika 12 alipoingia hekaluni, na siyo tu kwamba alikuwa anawasikiliza waalimu, lakini pia alikuwa anawauliza maswali. Msitari wa 47 inasema wote walishangazwa na uelewa wake na majibu yake.

Kila mmoja wetu na aseme kuwa tupo katika kufanya kazi ya Baba?

Yesu alijulikana kama mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Yohana 3:1-2, "*Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo mkuu wa Wayahudi. Huyo alimjia usiku akamwambia Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*"

Nikodemo alikuwa mmoja wa wakuu wa makuhani, na baadaye akaongea akimtetea Yesu (Yohana 7:45-52), na pia alikuwa mmoja wa waliouandaa mwili wa Yesu baada ya kusulubiwa kwa mapaundi ya myrrh na aloe. Yawezekana alikuja kwa Yesu usiku kwa sababu wakuu wa Kiyahudi wote hawakuwa wakweli. Nikodemo akakiri kwamba alikuwa mwalimu aliyetoka kwa Mungu kwa sababu hakuna mtu awezaye kufanya miujiza aliyofanya isipokuwa Mungu alikuwa pamoja naye.

Neno la msingi tunaloweza kupata ni ukweli kwamba Yesu alikuwa anahubiri. Miujiza aliyoifanya inathibitisha mambo aliyosema kuwa ni kweli.

Yesu Anatutaka Kuwatafuta na Kuwaokoa Waliopotea, Pia.

Mat. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenye, ajitwike msalaba wake, anifuate.*"

Ubebaji wa msalaba kwa upana wake hueleweka vibaya. Sio karne ya zamani, umasikini. Ushuru, magonjwa, hewa mbaya, au kitu chochote ambacho huvunja moyo katika maisha. Ni kukubalika kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, kwa baadhi ya mzigo au mizigo ichukuliwayo nje ya matakwa ili kutimiza mapenzi ya Mungu.

Wakristo wengi wamepokea dhihaka kwa sababu ya kueleza mapenzi ya Mungu. Hawakujiuzulu katika kuhubiri Injili eti kwa sababu tu wengine waliwaambia kuwa imara, au kuacha kufundisha katika jina hili la Yesu.

Mdo. 5:27-29, "*Walipowaleta wakawaweka katika baraza. Kuhani mkuu akawauliza, akisema, je! Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa jina hili? Nanyi tazameni mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu na mnataka kuileta damu ya mtu yule juu yenu. Petro na mitume wakajibu, wakisema imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.*"

Ni agizo lipi la Mungu ambalo Petro alikuwa akilizungumzia?

- Marko 16:15-16, "*Akawaambia **enendeni** ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

- Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi **enendeni** mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa* dahari.

Hakuna ambacho kingeachwa kuhusu kufundisha maagizo ya Mungu.

Je ilikuwa sawa kukataa agizo hili?

1 Kor. 9:16-17, "*Maana japokuwa naihubiri injili sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili. Maana nikiitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu, ila ikiwa si kwa hiari yangu, nimeaminiwa uwakili.*"

Paulo, katika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo, alimsii asilegee katika kuihubiri Neno la Mungu.

1 Tim. 4:13, "*Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha.*"

Mara nyingi nanywea ninaposikia mtu anasema, "Hatumuongoi mtu kwa kukariri Neno la Mungu katika koromeo zao, hivyo tunafundisha kwa mifano." Tunafundisha kwa mifano, lakini hatuwezi kuishia hapo. Inapaswa kuwa na hatua ambapo Neno la Mungu linawakilishwa.

Kumbuka, Paulo alisema, "*Ole wangu nisipoihubiri Injili!"*

Usiuze Injili kiulaini, na usiombe msamaa kwa Injili. Iwakilishe.

Wengine wanakuwa kama wanaonea haya mpango wa Mungu wa kuwaokoa walipotea, na kujaribu kuleta mawazo ili kuwafikia watu kwa mfumo wao wenyewe.

- Rum. 1:16-19, "*Kwa maana siionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani. Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi*

wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu. Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia."

- 1 Kor. 1:18-21, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuuzi wa lile neno linalohubiriwa.*"

Neno la Mungu linaweza kuwakilishwa katika mpangilio uliomzuri bila kuwa mzigo na kuwakimbia wengine.

Dhumuni letu linapaswa kuokoa nafsi za watu.

Wote tunaweza kuangalia mifano jinsi baadhi ya watu waliovyokwazwa kwa jinsi ambavyo baadhi ya watu walivyowakilisha maandiko kwao. Hii haimaanishi kwamba kuihubiri injili sio mfumo ambao unaweza kutumika. Kumbuka, kuihubiri injili ni mfumo wa Mungu kwa wokovu. Inampendeza Mungu kwamba mfumo huu unatumiwa.

Wengine wataudhiwa. Kila wakati ambapo haiepukiki.

Kristo alisema wengi watachukiwa kama wangemfuata na kuihubiri Neno lake.

- Yohana 17:14-17, "*Mimi nimewapa neno lako, na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*"

- Yohana 15:18-22, "*Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile neno nililowaambia, mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi, ikiwa walilishika neno langu, watalishika na lenu. Lakini haya yote*

watawatenda kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyenipeleka. Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi, lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao."

- 2 Tim. 3:12, "*Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utumwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.*"

Tunaona Kanisa La Kwanza Likiwatafuta Waliopotea.

- Roho 3000 ziliokolewa Siku ya Pentekoste kwa mahubiri ya Petro. Mdo. 2:37-41, "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na watu waote watakaitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"

- Mdo. 8:4, "*Lakini wale waliokusanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno.*"

- Mdo. 20:20, "*Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba.*"

- Mdo. 5:42, "*Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.*"

- Mfano wa Filipo akimfundisha Towashi. Alimbatiza siku hiyo hiyo. Mdo. 8:26-39, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda gaza nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda mara akamwona mtu wa Kushi, towashi mwenye mamlaka juu ya kandake Malkia wa kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya, akanena, je yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsii Filipo*

apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema nakuomba, nabii huyu anasema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akfunua kinywa chake naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini; Filipo na yule towashi naye akambatiza. Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena, basi alikwenda zake akifurahi."

- Mfano wa Anania akimfundisha Paulo alichopaswa kufanya ili aokolewe. Mdo. 22:6-16, "*Ikawa nilipokuwa nikisafiri, nikakaribia Dameski, wakati wa adhuhuri, ghafla nuru kuu alitoka mbinguni, ikanimulika pande zote. Nikaanguka nchi, nikasikia sauti ikiniambia, Sauli, Sauli mbona unaniudhi? Nikajibu wewe u nani Bwana? Akaniambia Mimi ni Yesu Mnazareti ambaye wewe unaniudhi. Na wale waliokuwa pamoja name waliuona ile nuru, lakini hawakuisikia ile sauti ya yule aliyesema nami. Nikasema nifanye nini, Bwana? Bwana akaniambia, simama, uingie Dameski na huko utaambiawa habari za mambo yote yaliyoamriwa uyafanye. Na nilipokuwa sioni kwa sababu ya fahari ya nuru ile, nikaongozwa na mikono yao waliokuwa pamoja nami, nikaingia Dameski. Basi mtu mmoja Anania, matauwa kwa kuifuata sheria aliyeshuhudiwa wema na Wayahudi wote waliokaa huko. Akanijia akasimama pamoja nami, akaniambia ndugu yangu Sauli, uone. Nikamwinulia macho yangu saa ile ile. Akasema, Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake na kumwona yule mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake. Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia. Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"

- Mfano wa Prisila na Akila wakimfundisha Apolo "*njia ya Mungu* kikamilifu *zaidi*". Mdo. 18: 24-26, "*Basi Myahudi mmoja jina lake*

Apolo, mzaliwa wa Iskanderia, mtu wa elimu akafika Efeso; naye alikuwa hodari katika maandiko. Mtu huyo alikuwa amefundishwa njia ya Bwana na kwa kuwa roho yake ilikuwa ikimwaka, alianza kunena na kufundisha kwa usahihi habari za Yesu, naye alijua ubatizo wa Yohana tu. Akaanza kunena kwa ujasiri katika sinagogi; hata Prisila na Akila walipomsikia wakamchukua kwao, wakamweleza njia za Bwana kwa usahihi zaidi."

Watu Wanahitaji Mwongozo; Mungu Anategeme Wakristo Kufanya Hili

Mdo. 8:30-31, "*Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, je yamekuelea haya unayosoma? Akasema, nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye.*"

Angali kwamba Filipo anachukua nafasi katika hali iliyopo ili kuwakilisha injili kwa Towashi. Hakutokea kama mtu aliyekuwa anachukuliana na maandiko alitumia maswali rahisi, na akakaribishwa ili akae na towashi ili waweze kulijadili zaidi. Hii inapaswa kuwa dhumuni letu, pia.

Wengine wataudhiwa kwa kile wanachokisikia. Lakini kama tukifanya kazi yetu kikamilifu, dhihaka yao itakuwa tu kwa sababu ya ujumbe ambao hawapendi, na sio kwa njia ambayo imetolewa.

Mvuvi havui samaki isipokuwa akitupa ndoano yake kwenye maji. Mat. 4:19, "*Akawaambia nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.*"

Ukristo ni ujuzi unaotenda kazi. Kristo ameeleza kwamba anataka wafuasi watakaozifanyia kazi nafsi za wengine.

Tuna Jukumu La Kila Mmoja Kutafuta na Kukiokoa Kilichopotea

2 Tim. 2:2, "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*"

Paulo alimfundisha Timotheo kwenda nje na kuwafundisha wanaume waaminifu nao pia kwenda nje na kufundisha wanaume waaminifu. Neno la Mungu linapaswa kuhubiriwa.

Fil. 2:15-16, "*Mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu wasio na hila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu,*

mkishika neno la uzima; nipate sababu ya kuona fahari katika siku ya Kristo, ya kwamba sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure."

Tusiposhikilia Neno la Mungu (kulihubiri), tutahesabiwa makosa.

Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*"

Yuda, katika waraka wake kwa ujumla kwa udugu, anawahimiza ndugu kuishindania imani kwa hakika. Hii haifanyiki kwa kukaa kimya na kuiacha neno lituangalie kuwa Wakristo wema. Hii ilikuwa ni kazi iliyo hai waliopaswa kufanya.

1 Pet. 3:15, "*Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu: mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.*"

Hii inahitaji kusoma na maandalizi. Wakati mwingine tunaweza kujikuta wenyewe hatupo tayari kujibu maswali fulani. Badala ya kutoa jibu ambayo inaweza ikawa sahihi au siyo sahihi, mjulishe muuliza swali kwamba ungependa kukutana nao ili mjadili swali. Alafu jifunze juu ya swali hilo, na uwe tayari kwa ajili ya mjadala. Mara baada ya kufanya hivyo, unapaswa kujiandaa wakati mwingine mtu akikuuliza swali kama hilo.

Fil. 1:14, "*Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kunena neno la Mungu pasipo hofu.*"

Paulo aliwekwa gerezani kwa sababu ya kuhubiri kwake. Kwa sababu ya jinsi alivyotenda (mjasiri, mpole, pasipo uoga, n.k), wengine walitiwa nguvu ili kutenda vivyo hivyo.

- Mdo. 16:20-33, "*Wakawachukua kwa makadhi, wakasema watu hawa wanachafua sana mji wetu nao ni Wayahudi; tena wanatangaza habari ya desturi zisizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata, kwa kuwa sisi tu Warumi. Makutano wote wakatoka wakawaendea, makadhi wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakatoa amri wapigwe kwa bakora. Na walipokwisha kuwapiga mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana. Naye akiisha kupata amri hii akawatupa katika chumba cha ndani, akawafunga mguu kwa mkatale. Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. Ghafla pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa. Yule mlinzi*

wa gereza akaamka, naye alipoona ya kuwa milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga akataka kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia. Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Usijidhuru kwa maana sisi sote tupo hapa. Akataka taa ziletwe akarukia ndani, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila; kisha akawaleta nje akisema, Bwana zangu yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake. Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao kisha akabatizwa, yeye na watu wake wakati uo huo."

- Kol. 4:5-6, "*Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati. Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.*"
- "*…Mkiukomboa wakati…*" ni neno linalomanisha "kuununua nafasi," ikichukua nafasi nzuri kwa matukio yote ya kutenda wema," n.k.
- "*…Maneno …yawe na neema…*" maneno yanayopendeza, huwekwa alama na utamu pamoja na hekima.
- "*…Yakikolea munyu…*" hutoa maneno yanayohitajika kutunza nafsi zao. Kwa watu wengine kunaweza kuwa na kasumba ya kuwalisha asali na chakula kitamu, lakini Paulo anatuambia kuwalisha chakula kitakacho sitawisha roho zao, na kuwa katika utekelezaji wa mwisho.

Jua jinsi ya kumjibu kila mtu.

Mungu atafanya sehemu yake. Naye anategemea na sisi tufanye sehemu yetu.

1 Kor. 3:6, "*Mimi nilipanda Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu.*"

Neno la Mungu ndilo linapswa kuwa na mvuto juu ya akili zao, sio kile tuancho dhani inaweza kuwa.

Watu Wanaosikiliza Neno Watatenda Tofauti

Haiwezi kuwa mara zote kwa sababu ya jinsi inavyotolewa. Kama wakilikataa Neno, usifanye kosa la kudhani, "Vizuri, nimekosea uwakilishaji." Watu wanaenda kutenda tofauti kwa Neno.

- Mat. 13:1-9, "*Siku ile Yesu akatoka nyumbani, akaketi kando ya bahari. Wakamkusanyikia makutano mengi, hata akapanda chomboni, akaketi na ule mkutano wote wakasimama pwani. Akawaambia mambo mengi kwa mfano, akisema tazama mpanzi alitoka kwenda kupanda. Hata alipokuwa akipanda mbegu zingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila; nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi, mara zikaota kwa udongo kukosa kina; na jua lilipozuka ziliungua na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. Zingine zikaanguka penye miiba, ile miiba ikamea, ikazisonga; nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa moja mia, moja sitini, moja thelathini. Mwenye masikio na asikie.*"

- Mat. 13:18-23, "*Basi ninyi sikilizeni mfano wa mpanzi. Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asilielewe nalo huja yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia. Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha; lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa. Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno; likawa halizai. Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyo ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo; yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu sitini, na huyu thelathini.*"

Sababu zimeenea ni kwa nini watu hawapokei Neno la Mungu. Sababu hizo kwa ujumla hazihusiani na Mkristo kuliwakilisha Neno. Inahusiana na jinsi msikilkizaji anavyopenda kulisikia Neno katika maisha yake.

Wengine Watatafuta Sababu Ya Kutokutafuta

Luka 14:16-24, "*Akamwambia mtu mmoja alifanya karamu kubwa akaalika watu wengi, akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, Njooni kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwa tayari. Wakaanza wote kutoa udhuru wote kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia nimenunua shamba sharti niende nikalitazame; <u>tafadhali unisamehe</u>. Mwingine akasema nimenunu ng'ombe jozi tano, , ninakwenda kuwajaribu, <u>tafadhali unisamehe</u>. Mwingine akasema, nimeoa mke na kwa sababu hiyo siwezi kuja. Yule mtumwa akaenda akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba*

akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Mtumwa akasema, Bwana hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa. Maana nawaambia katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu."

Kila mmoja wao alitoa udhuru ulioonekana ni nzuri kwao, lakini udhuru huu haukukubaliwa na Bwana.

Wengine Wanaangalia Majira Yanayowezekana

2 Tim. 4:2, "*Lihubiri neno, uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea kwa uvumilivu wote na mafundisho.*"

Wakati mwingine nafikiria katika akili yangu, "Nimetingwa sana kufanya hili kwa sasa. Nitasubiri hadi nitakapopata muda mwingi kwa kazi ya Bwana." Kama tukiendelea kuweka kazi zetu pendeni, hazitafanyika. Tunatakiwa kupata muda ili kuweka kazi ya Bwana mbele kuliko zetu.

Kulihubiri Neno ni Kazi Njema. Nini Kinatokea Kama Tusipoitenda?

Ni dhambi.

Yakobo 4:17, "*Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.*"

Sio aminifu.

1 Thes. 2:4, "*Bali kama vile tulivyopata kibali kwa Mungu tuwekewe amana Injili, ndivyo <u>tunenavyo; si kama wapendezao wanadamu</u>, bali wampendezao Mungu anayetupima mioyo yetu.*"

Inashindwa kuzaa matunda.

Yohana 15:1-8, "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondo; na kila tawi lizaalo hulisafisha ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. <u>Kaeni ndani yangu</u> nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana maana pasipo mimi ninyi*

hamwezi kufanya neno lo lote. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu."

Itasababisha wengine kupoteza roho zao.

- Yakobo 5:20, "*Jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhami.*"
- Ezek. 3:18-21, "*Nimwambiapo mtu mbaya hakika atakufa, wewe usimpe maonyo wala, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya kusudi aache njia yake mbaya na kujiokoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Lakini ukimwonya mtu mbaya , wala yeye hauachi ubaya wake, wala njia yake mbaya, atakufa katika uovu wake; bali wewe umejikoa roho yako. Tena mtu mwenye haki aiachapo haki yake na kutenda uovu, nami nikiweka kikwazo mbele yake, atakufa kwa sababu hukumwonya, atakufa katika uovu wake, wala matendo yake ya haki aliyoyatenda hayatakumbukwa; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Bali ukimwonya mwenye haki, kwamba yule mwenye haki asitende dhambi, tena ikiwa yeye hatendi dhambi, hakika ataishi, kwa sababu alikubali kuonywa nawe umejiokoa roho yako.*"

Hitimisho

Hivyo tafuta na uwashawishi wengine.

2 Kor. 5:11, "*Basi tukiijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu; lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu. Nami natumaini ya kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zetu pia.*"

Mashamba ni meupe.

- Yohana 4:35, "*hamsemi ninyi, bado miezi mine, ndipo yaja mavuno? Tazama mimi niwaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno.*"
- Mat. 9:37, "*Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache.*"